

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

610


UALIMU

Muda: Saa 3


Jumatatu, 07 Mei 2018 asubuhi

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E zenye jumla ya maswali **kumi na nane (18)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na swali **moja (1)** kutoka katika kila sehemu B, C, D na E.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B, C, D na E zina alama **kumi na tano (15)** kila moja.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



1



SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Bainisha faida nne kwa mwalimu kujifunza Saikolojia ya Elimu.
2. (a) Eleza kwa kifupi maana ya mtaala.
(b) Andika kwa kifupi aina kuu tatu za mtaala.
3. Bainisha madhumuni manne ya ufundishaji na ujifunzaji wa Elimu ya Watu Wazima katika mpango wa Kisomo Chenye Manufaa na Kisomo cha Kujijendeleza.
4. (a) Eleza kwa kifupi maana ya mfiko katika Upimaji wa Kielimu.
(b) Chunguza alama zifuatazo: 88, 80, 70, 60, 54 na 50 na kisha jibu maswali yanayofuata:
 - (i) Kokotoa wastani.
 - (ii) Tafuta mfiko.
 - (iii) Toa tafsiri ya jibu la mfiko ulilopata kwenye swali la 4 (b) (ii).
5. Orodhesha mambo manne yanayoweza kumsaidia mwanafunzi kuhawilisha maarifa.
6. (a) Unaelewa nini kuhusu dhana ya Elimu Jumuishi?
(b) Taja makundi matatu ya wanafunzi ambao wanafaa kuingizwa katika darasa la elimu jumuishi.
7. Bainisha hatua nne ambazo mwalimu wa somo anaweza kuzifuata katika kuwasaidia wanafunzi wenye utovu wa nidhamu darasani ili waweze kufaidika na mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.
8. Orodhesha majukumu manne ya Kamati ya Nidhamu katika shule za msingi.
9. Eleza kwa kifupi sababu nne za kuwepo kitengo cha ushauri na unasihi katika shule za msingi.
10. (a) Toa sababu moja ya kurekebisha makasi za wanafunzi baada ya kusahihisha mitihani yao.
(b) Rekebisha kwa kigezo cha T alama ya mwanafunzi aliyepata 75% katika darasa lenye wastani wa 45 na achano sanifu la 15.

SEHEMU B: SAIKOLOJIA YA ELIMU (Alama 15)

Jibu swali **moja (1)** kutoka katika sehemu hii.

11. Bainisha hatua za ukuaji wa mtoto kulingana na mwanasaikolojia Jean Piaget. Eleza wazi umuhimu wa kielimu kwa kila hatua husika.
12. Familia na jamii wana wajibu wa kuendeleza makuzi ya mtoto kimwili, kiakili na kijamii. Jadili mambo sita yanayotakiwa kufanywa na familia ili kufanikisha makuzi bora ya mtoto.

SEHEMU C: MITAALA NA UFUNDISHAJI (Alama 15)

Jibu swali **moja (1)** kutoka katika sehemu hii.

13. Eleza mambo muhimu sita ya kuzingatia katika ufundishaji wa darasa mseto.
14. Tumia hoja sita kupendekeza utaratibu unaofaa katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia filamu kama zana/kifaa cha kufundishia.

SEHEMU D: UTAFITI WA KIELIMU, UPIMAJI NA TATHMINI (Alama 15)

Jibu swali **moja (1)** kutoka katika sehemu hii.

15. Eleza hatua sita muhimu zinazotakiwa kufuatwa wakati wa ujaribishaji na urekebishaji wa zana za utafiti.
16. Bainisha vipengele muhimu vya kuzingatia wakati wa kuandika ripoti ya utafiti wa kielimu kuanzia sura ya kwanza mpaka ya sita.

SEHEMU E: MISINGI YA ELIMU (Alama 15)

Jibu swali **moja (1)** kutoka katika sehemu hii.

17. Kwa kutumia hoja sita, fafania kuhusu kazi za Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania (TSD).
18. Eleza mambo muhimu sita yaliyosisitizwa katika mpango wa pili wa miaka mitano (1969 - 1974) wa maendeleo ya elimu nchini Tanzania.